**USAFIRI**



# Mkakati huduma ya daladala baada ya mwendokasi

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Katikati ya dhana kuwa kuimarika kwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) kutawaathiri wamiliki wa daladala, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Udart), umesema tayari utaratibu maalumu umepangwa kuhakikisha biashara ya wasafirishaji hao haiathiriki.

Mtendaji Mkuu wa Udart, Dk Athumani Kihamia alisema utekelezwaji wa utaratibu huo, utahusisha kuundwa kwa kampuni ili daladala zote ziwe katika mfumo rasmi, badala ya ilivyo sasa kila daladala ikinunuliwa inatafuta njia yake.

Hata hivyo, wakati mradi wa awamu wa kwanza ulipokaribia kuanza kazi, kwa mujibu wa wamiliki wa daladala mkoani utaratibu uliotumika kuwaondoa ulihusisha mwekezaji aliyelipa fidia ya Sh4 milioni kwa kila daladala iliyokuwa inafanya kazi katika njia hiyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Chama cha Wasafirishaji Mkoa wa Dar es Salaam (Uwadar) kipindi hicho, Gharib Mohamed alisema katika fedha hizo walikubaliana Sh3 milioni walipwe moja kwa moja na Sh1milioni iliyobaki ziingizwe kwenye umiliki wa hisa wa Kampuni ya Udart wakati huo, ikiwa chini ya mwekezaji Robert Kisena.

Jingine walilokubaliana Mohamed alisema ni kuundwa kwa kampuni zinazotokana na wamiliki wa daladala zilizotoa Kampuni ya Uwadar na Kampuni ya Wazawa, lengo likiwa kuwa miongoni mwa wawekezaji watakaoleta mabasi yao katika mradi huo, lakini mwisho wa siku hilo halikufanikiwa.

"Kipindi kile kulikuwa na ushirikishwaji wa hali ya juu kati yetu wamiliki wa daladala, Dart na mwekezaji, tofauti na sasa mambo mengi tunayasikia tu huko mitandaoni au kusoma kwenye magazeti kama watu wengine lakini sio wadau muhimu katika usafirishaji," alisema Mohamed.

Akizungumzia hilo juzi katika mahojiano maalumu na *Mwananchi* alisema: "Wakishaunda kampuni ndio sasa wanamiliki hizo daladala watakazokuwa na hisa kulingana na wingi wa daladala alizonazo mtu na baada ya hapo, Serikali inatarajia kufanya uwezeshaji ikiwamo mafunzo na kuwapatia mikopo ya kununua magari mengi zaidi."

Wakati kwa upande wa madereva, alisema hilo watafaidika nalo kwa kuwa wataanza kulipwa mishahara tofauti na sasa hivi, mtu akichukua daladala jioni anapeleka hesabu kwa tajiri.

"Dereva huyu hatujui siku ambayo hajapata au kapigwa faini; na kosa labda ni gari, anafukuzwa kazi na wakati huo ana familia inamtegemea kupitia kazi hiyo," alisema Dk Kihamia.

Katika kulitekeleza hilo, alisema wanashirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) na Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Rais Tamisemi, ingawa vinara wakubwa hapa ni Dart, ili kuhakikisha hilo jambo linafanikiwa.



"Hili lipo kwenye mipango yetu ya kibajeti na kimipango, kwa hiyo kabla ya mwisho wa mwezi huu tutakutana na wamiliki wa daladala na madereva ili tuweze kujadiliana namna bora ya kuweza kutekeleza hilo.

"Maana kwa kuwashirikisha tu wamiliki peke yao wanaweza wakaelewa wachache na wengine wakabaki kushangaa, kwa sababu pia tumegundua wamiliki wa daladala ni watu wengine kabisa, na watumishi ni wengine, kwa hiyo waathirika wakubwa si wamiliki bali ni madereva na makondakta wao," alisema.

Hata hivyo, alikiri kila mabadiliko mwanzoni huwa yakitiliwa shaka lakini hayaana uhakika asilimia 100 madereva watakuja kunufaika wao na kuahidi kwamba, mwanzoni wanasaidiwa mpaka pale watakapoona wameweza kusimama wenyewe kwani watawasaidia hadi kifedha ili kuunda kampuni hizo.

Alisema kwa kuwa katika mradi huo wa mwendokasi mabasi yao hayatahusika kabisa, lakini kupitia mradi wa ujenzi wa barabara za DMDP zilizotengewa zaidi ya Sh1 trilioni, ana uhakika watapata maeneo ya kupeleka magari yao na mpaka zitabaki.

Alipoulizwa kuhusu kampuni zilizoundwa katika awamu ya kwanza kama zinaweza kutumika, Dk Kihamia alisema kama itawapendeza kuendelea nazo, itakuwa sawa kwao kama wataona wafungue nyingine nayo heri.

> **"Dereva huyu hatujui siku ambayo hajapata au kapigwa faini; na kosa labda ni gari, anafukuzwa kazi na wakati huo ana familia inamtegemea kupitia kazi hiyo."**
>
> Dk Kihamia

Kwa kufanya hivyo pia alisema wataweza kukopesheka na tayari benki mbalimbali zimeonesha nia ya kukubali hilo na siku moja huenda nao, wakamiliki mabasi yao ya mwendokasi yanayoweza kutumika kuchukua abiria kutoka pembezoni na kuwapeleka barabara kuu.

"Vilevile tayari wafadhili mbalimbali wanaofadhili Serikali katika miradi mbalimbali ya usafiri wameshakubali kufadhili hilo na sasa mshauri mtaalamu wetu yupo kazini kutengeneza baadhi ya vipengele, kimojawapo ni namna bora ya daladala zitaendeshwa na akimaliza atatupatia ripoti yake," alisema.

### Walichosema wamiliki, madereva

Wakitoa maoni yao kuhusu hatua hiyo, baadhi ya wamiliki wa daladala na madereva walisema, ni jambo zuri kwa kuwa ndio ilikuwa ndoto zao za siku nyingi.

"Tulishatoa kilio chetu hiki kuwa nasi tunataka kuwa moja ya wawekezaji katika mradi huo, lakini ikawa kama kilio cha samaki maji kwenda na maji, hivyo kama Serikali imeona hili lina tija kwa sasa tunashukuru,"alisema Break Salim mmoja wa wamiliki wa daladala.

Salim alisema wapo tayari kuwa wawekezaji katika mradi huo huku akiomba wapewe njia moja hata ya majaribio ili Serikali ione kama watashindwa.

Aliyewahi kuwa Mwenyekiti na Mwanzishi wa Uwadar, Ghalib Mohammed alisema kwa kuwa wamebaini madhaifu hayo na kutaka kuyarekebisha wanawasubiri siku wakiitwa watatoa maoni yetu.

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Madereva Dar es Salaam (Darcoboa), Sabri Mabrouk alisema katika utekelezaji wa mradi huo, kikubwa wamiliki wanatakiwa kubadilika kuendana na wakati kwa kuwa, katika safari hiyo ya usafirishaji wamepita katika hatua mbalimbali.

"Katika kazi hii ya kutoa huduma za usafiri tumepita katika hatua mbalimbali kuanzia gari aina ya cha maharagwe baadaye Hiece maarufu vipan[illegible] DCM Tata na Hier na sas[illegible] hivyo hatuwezi kus[illegible] ni kukubali kubadilika kuendana na wakati," alisema Mabrouk.

Mwenyekiti wa Umoja wa Madereva na Makondakta Mkoa wa Dar es Salaam (Uwamada), Shukuru Mlawa alisema wao wapo mguu sawa kuanza kwa huduma hizo.

Mlawa alisema katika kupata ajira kwenye mradi huo au kampuni zitakazoundwa kama wanavyosema Dart, kila dereva anahitaji, kwa kuwa kazi ya daladala ni ngumu na wanatumia nguvu kubwa katika kufanikisha hesabu za matajari wao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi Madereva Tanzania(Tadwu), Ally Kimaro alisema suala la mikataba kwa madereva sio jambo geni, kwa kuwa lilishaundiwa na ilipopotelea hawajui.

Kimaro alisema mpaka hapa walipo migogoro ni mingi na hawajui Dart watakuja na sera gani, kwa kuwa hata wizara yenye dhamana na kazi imeshindwa kutatua changamoto hiyo.

"Ushauri wangu kwa sasa katika suala la madereva, zitakapoundwa kampuni wanazozisema ili kuwapa afueni madereva kuwa na mikataba, lakini pia kwa hizo za mwendokasi zitakapoanza kufanya kazi wizara ya kazi ikae mbele kuhakikisha hilo linatekelezeka kivitendo.

"La sivyo, danadana zitakuwa ni zilezile na ukizingatia madereva walivyo mtu ukiacha kazi leo, mwenzako kesho anaenda kufanya kazi hiyohiyo kwa ujira mdogo,"alisema mwenyekiti huyo.

Hata hivyo, alisema wakati kima cha chini cha mshahara kilichopangwa na Serikali kikiwa ni Sh300,000 pamoja na marupurupu mengine ikiwamo huduma za afya na nauli lakini ukweli ni kwamba, kuna wamiliki hata Sh200,000 ya mdomo kulipana na madereva wao kwa mwezi ni kazi.

CamScanner

Nukuu



"Kuna mtu amekaa kwe
aliupanda mti miaka mi

Warren Buffet, mfanyabi

# Huduma ya mwendokasi Mbagala isichelewe

Kwa muda mrefu sasa, wakazi wa Mbagala na maeneo ya jirani wamekuwa wakisubiri kwa hamu huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka, maarufu kama mwendokasi.

Ni mradi ambao kwa muda mrefu umekuwa ukiishi kwenye maneno, ahadi na matarajio, huku miundombinu ya kisasa ikiwa tayari imesimama kama ushahidi wa kile kinachotakiwa kuwa suluhisho la muda mrefu kwa tatizo la usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Katika mazingira haya, ni vigumu kulaumu wananchi wanaosema, "tusubiri tuone" badala ya kushabikia tangazo jingine la kuanza kwa huduma hiyo.

Hii ni kwa sababu matarajio yamekuwa yakipandishwa kwa ahadi kubwa, lakini utekelezaji wake ukicheleweshwa hadi matumaini yanapogeuka malalamiko.

Wakazi wa Mbagala hawahitaji tena maneno mazuri, wanahitaji kuona mabasi ya mwendokasi yakianza kazi, kwa wakati, kwa ufanisi na kwa mfumo unaozingatia uhalisia wa maisha ya watu wanaohitaji huduma hiyo kila siku.

Kampuni ya Mofat, iliyopewa jukumu la kuendesha awamu hii ya pili ya mradi wa wa mabasi yaendayo haraka (BRT) kupitia Barabara ya Kilwa (Mbagala), imeonesha nia na mikakati ya kujibu changamoto zilizoonekana kwenye awamu ya kwanza, hususan kwenye Barabara ya Morogoro.

Hilo ni jambo la kupongezwa, kwa kuwa hali ya sasa ya usafiri inahitaji zaidi ya magari, inahitaji mifumo, nidhamu na huduma inayoweka abiria mbele.

Kwa sasa, hali ya usafiri kuelekea maeneo ya Mbagala na pembezoni kama vile Chanika, Kisemvule, Mbande, Chamazi, na Rufiji imekuwa ya kusikitisha. Gari za kwenda Kariakoo au katikati ya jiji ni haba, na nyingi hufika zikiwa tayari zimejaa.

Wafanyabiashara, wanafunzi, wafanyakazi wa sekta mbalimbali na hata kinamama wanaokwenda hospitalini wamekuwa wakikumbana na hali ya kero isiyostahili katika jiji linaloelekea kuwa mji wa kisasa.

Hii inafanya mradi wa mwendokasi kuwa si tu mradi wa usafiri, bali hitaji la kijamii na haki ya kimsingi ya kila raia wa eneo hilo.

Hata hivyo, Serikali kupitia Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dart) imeonesha dhamira ya kuhakikisha changamoto za awamu ya kwanza hazijirudii.

Lakini dhamira hiyo haitatosha iwapo hakutakuwa na ufuatiliaji wa karibu, uwazi katika utekelezaji, na uwajibikaji wa pande zote. Ni wakati sasa wa kusema ukweli, wakazi wa Mbagala wamevumilia vya kutosha. Miundombinu ipo, pesa zimetumika na watu wanasubiri tu mabasi yaingie barabarani.

Ndiyo maana tunasisitiza, usafiri huu uanze kwa wakati uliopangwa. Hakuna tena nafasi ya kusogeza mbele tarehe au kutoa sababu mpya. Tunashauri kuwa, mpango wa awamu hii ufuatiliwe kwa karibu na vyombo husika ili kuhakikisha kuwa unatekelezwa kwa uwazi na kwa manufaa ya umma.

Matatizo ya usongamano, uhaba wa magari, na ukosefu wa nidhamu ya huduma lazima yazuiwe kabla hayajawa sugu.

Tunaamini kuwa, iwapo Mofat itatekeleza mipango yake kama ilivyoahidi, na kama mabasi hayo yataanza kazi kama ilivyotangazwa, basi Mbagala itashuhudia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii. Huduma bora ya usafiri ni kichocheo cha maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa jumla. Ndiyo maana hatuwezi kuendelea kukubali ahadi zisizotekelezwa.

CamScanner

Habarileo Ijumaa Julai 11, 2025 Pg 2

# CCM yataka SGR bandari za Tanga, Mtwara

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema katika miaka mitano ijayo kitaelekeza uanze ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) itakayounganisha Bandari ya Tanga kwenda Arusha.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025-2030 imeeleza reli hiyo itafika Musoma ikiwa ni urefu wa kilometa 1,108 na itaungana na SGR ya kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma.

Pia, katika ilani hiyo CCM imeeleza itaelekeza serikali yake ianze ujenzi wa SGR kutoka Bandari ya Mtwara hadi Mbamba Bay wilayani Nyasa.

CCM imeeleza reli hiyo itakuwa na tawi la kutoka Songea hadi Ludewa ili kuunganisha na mradi wa makaa ya mawe (Liganga) na madini ya chuma (Mchuchuma).

Chama hicho pia, kitaelekeza ukamilishwe ujenzi wa SGR kwa kipande cha Mwanza – Isaka kilometa 341, Makutupora – Tabora kilometa 368, Tabora – Isaka kilometa 165, Tabora – Kigoma kilometa 506 na Uvinza – Musongati kilometa 156.6.

"Ujenzi wa miradi ya reli utapewa kipaumbele kwa reli ambazo zinafungua nchi kwa ajili ya biashara ili kutumia vizuri fursa ya kijiografia ambayo Tanzania inayo," imeeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2025 - 2030.

Pia, imeeleza kitaelekeza ijengwe reli na kuweka usafiri wa treni za mijini katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma ili kupunguza msongamano na kurahisisha usafiri.

Imeeleza CCM itaelekeza uimarishwe uendeshaji wa Reli ya Kati na Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kwa kuendelea na ununuzi wa vifaa vya uendeshaji wa reli ikiwamo vichwa vya treni, mabehewa, mitambo na mashine za matengenezo ya njia.

Mbali na hilo, itaelekeza ijengwe SGR kutoka Itigi hadi Singida na kijengwe kituo cha reli na mtandao wake ndani ya Bandari ya Dar es Salaam.

Ilani imeeleza CCM itaelekeza ikamilishwe miundombinu ya usafirishaji wa shehena za mizigo kupitia SGR na kuhamasisha matumizi yake.

Kuhusu bandari, CCM imeeleza katika miaka mitano ijayo itaielekeza serikali ijenge bandari mpya ya Bagamoyo na ijenge miundombinu ya bandari itakayounganisha Mkoa wa Kusini Unguja (Zanzibar) na Bagamoyo (Tanzania Bara).

Chama hicho kimeeleza kitaielekeza serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi ishiriki kuendeleza na kuendesha bandari nchini.

Pia serikali itaelekezwa iboreshe bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Kalema, Musoma na bandari kavu katika eneo la Kurasini - Dar es Salaam, Kwala - Pwani na Ihumwa – Dodoma.

"Tanzania ni lango la usafirishaji wa bidhaa kwa nchi saba ambazo hazikupitiwa na ushoroba wa Bahari ya Hindi. Hii ni fursa ambayo nchi inapaswa kuendelea kuitumia katika kukuza uchumi na kuimarisha mahusiano na kujipambanua kidiplomasia katika ukanda wa Afrika na duniani," imeeleza ilani hiyo.

CCM imeeleza itaielekeza serikali ijenge miundombinu ya kupokelea na kuhifadhi mafuta bandarini yenye mita za mraba 420,000.

Pia, chama hicho kitaelekeza [illegible] wa gati la kuhudur[illegible] mafuta lenye uw[illegible] mpaka [illegible] kwa wakati mmoja.